# JUNGU KUU LIMEISHA UKOKO? UENDELEZAJI WA KISWAHILI KUPITIA UUNDAJI WA MSAMIATI

***Sangai Mohochi***
**Idara ya Lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya**

**Ikisiri**
*Lugha ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii yoyote. Wakati huohuo, lugha ni kifaa muhimu cha kuueleza na kuendeleza utamaduni wa jamii husika. Kwa jumla, binadamu asingefikia kiwango cha maendeleo alicho nacho hivi sasa bila lugha. Kwa sababu ya uhusiano wa karibu baina ya lugha na utamaduni wa jamii, mabadiliko katika utamaduni wa jamii mbalimbali husababisha lugha kukuzwa ili kuyakidhi mahitaji mapya ya jamii. Kutokana na hali ya utandawazi, jamii mbalimbali ulimwenguni zinatangamana zaidi na kunakuwepo uhitaji wa kuunda msamiati wa kuzieleza dhana mpya zinazoibuka na kusambaa ulimwenguni kote kwa haraka zaidi. Makala haya yanajadili uundaji wa msamiati kama njia moja muhimu ya kuiendeleza lugha ya Kiswahili na kuifanya itutumikie katika karne hii mpya ya maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia. Inaonya kuwa, katika harakati hizo za kuiendeleza lugha, ni muhimu kufanya tahadhari ili tusiishie kuchukua maneno ya kigeni na kuyaswahilisha kiholela bila kuzingatia kwanza maneno ya kiasili yanayoweza kuzieleza dhana hizo barabara. Huo ndio utaratibu ambao baadhi ya wataalamu wa Kiswahili wanaufuata. Bila kufanya hivyo, tutaupoteza utamu wa Kiswahili tunaojivunia.*

## UTANGULIZI

Kote ulimwenguni, juhudi nyingi zimeelekezwa katika ustawi wa lugha. Hata hivyo, hili halijitokezi katika viwango sawa; zipo jamii ambazo zimelipatia swala la uendelezaji wa lugha kipaumbele kuliko nyingine. Mwaro (2000), anasema harakati hizi zina msingi wake katika umuhimu wa kuimarisha mawasiliano baina ya mataifa yanayotumia lugha tofautitofauti. Aidha, hili litasaidia kupatikana kwa maelewano ya lugha kitaifa na kimataifa. Miongoni mwa nchi ambazo zimejishughulisha kuendeleza lugha zao za kitaifa kileksoni ni: Uswidi, Ujapani, Uchina, Somalia, Israeli, India, na Ujerumani. Upande wa lugha ya Kiswahili, japo nchi mbalimbali ikiwemo Kenya, na Uganda zimetoa mchango mkubwa, ni Tanzania ambayo imeonyesha kuwa tayari zaidi kutumia raslimali ya umma katika kuiendeleza lugha hii. Katika mataifa yote yaliyotajwa, pamoja na mengine mengi, uendelezaji wa lugha ni ajenda muhimu ya kitaifa ambayo hutengewa fungu maalumu la fedha. Kufanikisha hili, mara

nyingi huwa kuna vyombo maalumuvilivyotwikwa jukumu hilo. Mfano mzuri ni mataifa ya Uingereza na Ufaransa ambayo kupitia kwa mashirika yao: *British Council* (Baraza la Wingereza), na *Alliance Francaise* (Ushirikiano wa Kifaransa) yamefanya bidii kuhakikisha kuwa lugha zao zinaendelea kushikilia nafasi muhimu kote ulimwenguni. Makala haya yanaelezea hali ya uundaji wa msamiati kama namna moja muhimu ya kuiendeleza lugha. Tatafafanua mbinu zilizotumika kimataifa kwa muhtasri, kisha yatachambua hali ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Suala kuu linalokusudiwa kupatiwa jibu linahusu ubora wa mkondo wa uundaji wa msamiati wa Kiswahili unaochukuliwa na baadhi ya wahusika. Makala haya yamechochewa na msimamo pamoja na mchango wa Marehemu George Aggrey Were-Mwaro (1968-2002) katika eneo pana la leksikografia. Lakini, tofauti na Mwaro (2000), ambaye katika tasnifu yake ya uzamifu amejikita zaidi katika uundaji wa istilahi kwa uwanda wa isimu, makala haya yanachambua msamiati wa lugha ya Kiswahili kwa ujumla wake.

**Uundaji wa Msamiati kama Njia Muhimu ya Ustawi wa Lugha**

Kutokana na ukweli kuwa lugha ina uhai na hubadilika kulingana na mabadiliko katika jamii, suala la msamiati mpya katika lugha ni la wakati wote, na hili ni kwa lugha zote ulimwenguni; kubwa kwa ndogo. Uundaji wa msamiati haufanywi kiholela bali kuna nadharia mbalimbali zinazofafanua kanuni na mbinu za uundaji wa msamiati. Katika makala haya, sitazama sana katika maelezo ya hizo nadharia za kileksikografia. Wapo wataalamu wengi wa eneo la uundaji wa istilahi za lugha ya Kiswahili ambao wameandika mengi kuhusu nadharia na mbinu za uundaji wa istilahi. Mwaro (2000) ametoa ufafanuzi mzuri kuhusu suala hilo, huku akiwarejelea magwiji wa eneo hili katika taaluma ya Kiswahili waliomtangulia. Miongoni mwa waliolijadili kuhusu umuhimu wa nadharia kuwa mhimili wa uundaji wa istilahi mwafaka ni Felber (1984), Mkude (1989), Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992), Mdee (1983), Massamba, (1989), na Massamba (1996). Nadharia kuu alizozirejelea Mwaro (2000) ni: Nadharia Jumla ya Istilahi (*General Theory of Terminology*) iliyoasisiwa na Eugine Wuster mwaka 1931; na Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (ya vigezo vya PEGITOSCA) iliyoasisiwa na K.B. Kiingi (1989).

Vivyo hivyo, lugha ya Kiswahili imelazimika kuwa mbioni kupata msamiati mpya ili kuyatosheleza mahitaji ya watumiaji wake. Kwa sababu hiyo, upanuzi wa msamiati wa Kiswahili umeshughulikiwa na mashirika mbalimbali na wataalamu binafsi, ndani na nje ya Afrika Mashariki kwa muda mrefu. Vyombo vikuu vinavyolishughulikia suala hili nchini Tanzania ni Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Kenya kuna chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA) na Baraza la Kiswahili la Kenya (BAKIKE), kwa kiwango kidogo. Vyombo hivi nchini Kenya vimetoa

mchango zaidi kutokana na juhudi za wanachama binafsi wala si kama asasi rasmi. Aidha, kuna mashirika yasiyo ya kiserikali, na waundaji istilahi binafsi. Hawa ni pamoja na Nabhany, Mbaabu na Chimerah. Nchini Tanzania kuna wataalamu wengi ambao wamejishughulisha na uundaji wa istilahi za Kiswahili kwa muda mrefu sana.

Kutokana na juhudi hizo za muda mrefu za wataalam na wapenzi wa lugha ya Kiswahili, lugha hii imeendelezwa na inatuwezesha kutekeleza shughuli muhimu katika taaluma na nyanja mbalimbali za maisha. Kwa mfano, Kiputiputi (1999) anaeleza kuwa, kwa mujibu wa BAKITA, istilahi 6000 zilikuwa zimeundwa kufikia wakati huo kwa matumizi ya sayansi, hisabati na teknolojia. Bila shaka idadi hiyo imeongezeka kufikia sasa kwani zoezi la uundaji wa istilahi ni la wakati wote. Aidha, kuna kamusi mbalimbali zilizochapishwa na TUKI, ikiwa ni pamoja na: *Kamusi Sanifu ya Biolojia Fizikia na Kemia*, *Kamusi ya Awali ya Sayansi na Teknolojia*, na *Kamusi ya Tiba*. Wote waliohusika wanahitaji kupongezwa na kuhimizwa kuzidisha juhudi. Hata hivyo, uundaji wa istilahi za Kiswahili umekumbwa na mjadala mkali na wa muda mrefu. Mjadala huo umetokana, miongoni mwa mengine, na ubora na ufaafu wa istilahi zinazoundwa, mbinu mwafaka zinazopaswa kutumiwa, pamoja na ukubalifu wa istilahi hizo. Hayo ndiyo masuala ninayoyageukia sasa katika sehemu zifuatazo za makala haya.

**Mbinu za Uundaji wa Istilahi**

Mbinu muhimu zilizotumika katika uundaji wa msamiati wa lugha ni unyambuaji, uambishi, uambatanishaji na uunganishaji, ufupishaji, uradidi, upanuzi wa maana za maneno, pamoja na ufufuaji na ujenzi wa mumo kwa mumo wa istilahi. Mwaro (2000) amezitolea ufafanuzi mrefu, ikiwa ni pamoja na kuzijadili kaidi zinazotawala mbinu mbalimbali, uzuri na upungufu wa kila mojawapo, pamoja na kutoa mifano ya msamiati uliozalishwa nazo. Katika lugha ya Kiswahili, mbinu hizi zimetumika kwa viwango vinavyotofautiana. Kwa ujumla, asasi na wataalamu binafsi wanaelekea kupendelea mbinu tofauti tofauti. Kwa sababu hiyo, zipo ambazo zimetumika zaidi zinapolinganishwa na nyingine. Katika kuzijadili mbinu mbalimbali za uundaji wa istilahi na kuzitathmini zilizobuniwa katika lugha ya Kiswahili, mjadala umejikita zaidi katika masuala makuu yafuatayo: kukubalika na kukataliwa kwa msamiati, umataifa wa istilahi, na lugha changizi inayopaswa kuzingatiwa.

**Kukataliwa kwa Msamiati**

Ni kweli anavyosema Mdee (1980), kwamba istilahi nyingi za Kiswahili zinazoundwa hukataliwa na wataalamu na watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa hakika, ni vizuri kutambua kuwa baadhi ya wataalamu wanakubali kuwa

istilahi za Kiswahili zina upungufu kwani bila kukubali kuwepo kwa tatizo si rahisi kulitafutia utatuzi. Mwingine ni Mwansoko (1990), ambaye pamoja na kukubali kuwepo kwa udhaifu huo, anasema kuwa istilahi hizo zinatumika kufundishia wanafunzi wa shule za upili, vyuoni, na chuo kikuu licha ya upungufu wake. Hali hii haibainiki katika nyanja ya elimu tu, bali pia katika matumizi ya kawaida na ya kila siku ya lugha ya Kiswahili. Nadhani kuna umuhimu mkubwa wa kujisaili kuhusu uundaji wa istilahi hizo. Wakati wote twapaswa kuzitathmini mbinu tunazozitumia ili kuziboresha na kuunda msamiati unaokidhi vyema zaidi mahitaji ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

Baadhi ya istilahi zinazoundwa na wataalamu wa Kiswahili zimekataliwa na watumiaji wa lugha hiyo kwa sababu ya kukosa 'usayansi' ama mwonjo (Temu 1984, na Khamisi 1987, wakitajwa na Mwaro, 2000: 2). Kuhusu usayansi, labda madai hayo yawe yanatolewa na wataalamu wa lugha. Watumiaji wengi wa lugha hawaelewi wala kulijali suala la usayansi wa msamiati. Kwa hakika, nadhani hawajui hata kuwa msamiati unapaswa kuwa na huo usayansi. Mwonjo ni sawa. Msamiati kukataliwa kwa sababu ya kukosa mwonjo ni mwitikio mzuri wa kuwawezesha wahusika kuyaangalia kwa makini hayo yaliyokataliwa. Maswali muhimu hapa ni, kwa nini yakakataliwa? Nini kifanywe kuyarekebisha na kuhakikisha kuwa hali hiyo inaepukwa katika siku za usoni? Ni jukumu la waunda istilahi za Kiswahili kufuata kanuni za kisayansi za uundaji wa istilahi (na hili lawezekana katika mbinu zote za uundaji wa istilahi bila kujali lugha changizi) na kuunda istilahi nzuri. Watumiaji wa lugha hawachunguzi usayansi wa msamiati kabla ya kuanza kuutumia.

**Suala la Lugha Changizi**

Suala la lugha changizi nalo limejitokeza mara nyingi katika mjadala wa uundaji wa istilahi za Kiswahili, na labda ndilo limezua mjadala mkali zaidi. Cha msingi hapa ni asili ya istilahi zinazobuniwa. Tubuni kutokana na lugha za kigeni au Kiswahili na lugha nyingine za kiasili? Mwansoko (Mwaro, 2000: 88), kwa mfano, anapendekeza lugha ya Kiingereza kwa sababu ndiyo lugha ambayo watumiaji wengi wa Kiswahili wametumia kupata elimu, na vitabu vingi vinavyotumika vimeandikwa kwa Kiingereza. Sidhani sababu hizi zinatosha. Kwanza, katika uendelezaji wa Kiswahili kwa jumla, tunawalenga wote wala si waliopata elimu tu (ambao ni wachache bado katika jamii). Pili, tulipokuwa tukipata hiyo elimu kwa Kiingereza, si tulizipata hizo dhana za Kiingereza zikiwa ngeni kwetu kabisa? Kwa nini Kiswahili kinapohusika ziegemezwe kwenye lugha nyingine kwa madai kuwa tayari tunaijua na kuitumia? Naye Abdulaziz (Mwaro, 2000:88-89), anapendelea Kiarabu kuwa lugha changizi kwa uundaji wa istilahi za Kiswahili kwa sababu ya maingiliano ya muda mrefu baina ya lugha hizo mbili. Ni kweli kuwa Kiswahili kimeingiliana kwa muda

mrefu na Kiarabu lakini hilo halitoshi kutufunga. Wapo wengi ambao wanaunga mkono, ama maoni ya Mwansoko au ya Abdulaziz. Ni muhimu tuchukue tahadhari isije ikawa tunarudi palepale kwa mvutano baina ya Waswahili asilia na jamii iliyo kubwa zaidi ya watumiaji wa Kiswahili kuhusu mkondo wa kuiendeleza lugha hii. Mfano mzuri wa mchuano huu ulijitokeza katika mgogoro wa ushairi wa Kiswahili.

Ilikuwa imependekezwa na BAKITA (Kakulu, 1982), kuwa suala la lugha changizi lizingatiwe katika uundaji wa istilahi za Kiswahili. Pendekezo hilo lililotolewa kwa kuangalia, kwanza Kiswahili chenyewe, lugha za Kibantu na lugha nyingine za Kiafrika, kabla ya lugha za kigeni ni zuri. Nakubaliana na Mwaro (2000), asemapo kwamba hili linawezekana (wakati wote tuliofundisha pamoja tulikuwa na mawazo sawa kwamba Kiswahili sharti kitunze uasili wake). Kwa kweli, ndiyo njia ya pekee ya kuhakikisha kuwa Kiswahili kinabakia kuwa Kiswahili, lugha ya Kiafrika. Msimamo wa Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992), kwamba kutokana na ukosefu wa utafiti wa kina kwa lahaja za Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika, lugha hizo haziwezi kutoa mchango kamilifu katika uendelezaji wa istilahi za Kiswahili unatetereka. Mbona kuna istilahi ambazo ziliundwa kutokana na lahaja na lugha nyingine za Kiafrika? Isitoshe, si utafiti unaomulika lahaja za Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika unaendelea na waweza kuzidishwa?

Huenda wakati mwingine baadhi ya wataalamu wa lugha hupungikiwa kwa sababu ya kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa lugha ya Kiswahili. Kwa hakika, hilo halipaswi, kamwe kuwa tatizo ama suala la kuonea aibu. Kiswahili si 'ugha ya mama'ya walimu na watafiti wengi wanaoishughulikia. Aidha, inaeleweka wazi kuwa, licha ya elimu ya muda mrefu, si rahisi kudai kuwa unaijua lugha maalum kikamilifu. Hata miongoni mwa Waswahili wenyewe, ufahamu wa lugha unatofautiana. Lakini wapo wazee wa Kiswahili wanaoifahamu lugha hii barabara. Kinachohitajika ni ushirikiano wa karibu baina ya wasomi, walimu, na wanaleksikografia wa Kiswahili na wazungumzaji wa lugha hii. Wala ushirikiano kama huo hautazuia matumizi ya nadharia na mbinu mbalimbali zinazoongoza uundaji wa istilahi mpya za Kiswahili na kuzipanulia matumizi zilizopo kwa kuzingatia mahitaji ya wakati huu. Isitoshe, kuutaka usaidizi wa Waswahili hakutatupunguzia uprofesa na utaalamu wetu hata chembe. Kwa nini tunapotaka kubuni istilahi zinazoambatana na nyanja maalumu ya taaluma kama vile, kemia, bayolojia, kompyuta na kadhalika, tunakubali kupata ushauri wa wataalamu wa nyanja hizo lakini inapokuja kwa wazungumzaji asilia wa lugha ya Kiswahili tunadhani hawana la kuchangia?

Kuegemea zaidi katika Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika kutasaidia kuijenga lugha ya Kiswahili katika misingi ya Kiafrika na wala si ya kigeni. Besha (1972:23, akinukuliwa na Mwaro, 2000:152) anasema hivi:

> Si lazima lugha ichukue maneno ya kigeni kila mara kunapokuwa na jambo jipya la kueleza. Maneno yenyewe ya lugha yanaweza kupanuliwa.

Aidha, Nkwera (1978) anapendekeza kuwa chemchemi au chimbuko la istilahi liwe Waswahili wenyewe. Tuanze na Kiswahili kisha lugha za Kibantu. Licha ya kuulinda Uafrika wa Kiswahili, kufanya hivyo kwaweza kutoa mchango mkubwa sana katika kuwadhihirishia wazi wapinzani kuwa Kiswahili ni lugha inayojitosheleza kikamilifu katika msamiati.

Wapo baadhi ambao suala hili la kupuuza uasili wa lugha ya Kiswahili na kukimbilia za kigeni linawakera sana. Kwa kweli, matamshi ya wengine yanaonyesha hasira na mihemko mikali mno. Mbega (1979, akinukuliwa na Mwaro, 200:1520), kwa mfano anasema hivi:

> Maneno karakhana (karakana), zahanati, kabaila, kipuri n.k. ni maneno ya wapi? Kwa nini tunakikuza Kiswahili kwa maneno ya kudondoza? Kwani tumechimbua ukale wa Kiswahili na kupata kuwa hatuna hazina ya maneno?...hiki si Kiswahili bali ni mpochongo wa maneno.

Ni kweli kuwa lugha ya Kiswahili inaingiliana na lugha nyingi tofauti, za kigeni. Aidha, kutokana na hali hiyo, na kwa kuzingatia kuwa uvumbuzi mwingi na dhana mpya zinatufikia kupitia lugha ya Kiingereza, haitawezekana kuepuka athari za Kiingereza na lugha nyingine za kigeni. Hata hivyo, hiyo si sababu inayotosheleza ya kuzikumbatia hizo lugha za kigeni hata pale ambapo zipo za kiasili.

Napendekeza kuwa, pale ambapo tayari maneno ya kigeni yametoholewa na kuswahilishwa kwa utaratibu mzuri kufikia hatua ya kukubalika na kutumika kwa mapana, tuendelee kuyatumia. Lakini tusite kukimbilia maneneo ya kigeni. Dhana mpya ziundiwe istilahi kwa kuzingatia lugha ya Kiswahili na lahaja zake mbalimbali. Kwa maana hiyo, msamiati wa Nabhany (1978) kama vile uhazigi (zahanati), udandi (penseli), mwiya (wakati), na matayo (lawama), japo wa kiasili, huenda usipate mashiko katika lugha ya Kiswahili kwa sababu hayo mengine yameishazoeleka. Ila mhusika huyu, pamoja na Waswahili wengine wajumuishwe katika uundaji wa istilahi za Kiswahili uhitaji unapozuka.

Ilivyo ni kuwa hakuna makubaliano kuhusu suala la lugha changizi katika harakati za kuundeleza msamiati wa Kiswahili. BAKITA (Kakulu, 1982), ilipendekeza vyanzo vifuatavyo:

1. Kiswahili chenyewe
2. Lugha za Kibantu
3. Lugha nyingine za Kiafrika
4. Lugha za kigeni.

Wataalamu wengine wametoa mapendekezo tofauti. Kwa mfano, Mwansoko (1989, 1990), ingawa anapendekeza Kiswahili chenyewe na lahaja zake, lugha za Kibantu, Kiingereza, Kiarabu, na Kigiritini (Kigiriki na Kilatini), anapendelea Kiingereza zaidi. Wanaopendelea Kigiritini ni pamoja na (Mdee, 1983: Mac William, 1985, na Kiingi (1989). Abdulaziz (1989) na Mwansoko (1990) wanapinga hoja ya Kigiritini. Kiarabu kama lugha changizi kina watetezi wengi pia (Akida 1977; Gibe, 1981, na Abdulaziz, 1985). Kulingana na Abdulaziz (khj.), yapaswa iwe lahaja za Kiswahili, Kiarabu, Lugha za Kibantu, na hatimaye Kiingereza na Kigiritini. Utaona kuwa amekiweka Kiarabu mbele ya lugha za Kibantu. Kwa jumla, "wanamkopo", ambao Mwaro (2000:161) anawaita watazama 'nje' ni wengi. Wengine ni pamoja na Likhako (1991), Mc Crum na wenzake (1986), Abdulaziz (1989), na Chimerah (1998). Moja kati ya sababu zinazotolewa kutetea msimamo huu ni ukweli kuwa ukopaji ni sifa ya lugha zote, na hata Kiingereza hukopa (inadaiwa kina asilimia 85% ya mikopo). Ati hiyo ndiyo sababu ya kujitosheleza kwa Kiingereza, na kwa sababu hiyo, hakuna haja ya 'kujisumbua', tufuate 'nyayo' za Kiingereza. Lakini, tumezingatia uwezekano kwamba Kiingereza kinakopa kiasi hicho kwa sababu hakina namna nyingine ya kupanua msamiati wake? Kwa mfano, hakina lahaja nyingi kama Kiswahili, wala lugha nyingi zinazokaribiana kimuundo na kimsamiati kama Kiswahili kilivyo na lugha nyingine nyingi za Kibantu.

Mjadala wa lugha changizi unafungamana na sifa ya umataifa wa istilahi. Kigezo cha umataifa kimetajwa kuwa muhimu sana katika uundaji wa istilahi (Felber 1984, katika Mwaro, 2000). Umataifa umedaiwa kuwa muhimu kwa sababu unarahisisha mawasiliano katika jamii zitumiazo lugha tofauti ulimwenguni, pamoja na kuwezesha ubadilishanaji wa maarifa na teknolojia na hivyo kusaidia kupunguza mwanya baina ya mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea. Siamini kuwa hilo ndilo litatutatulia tatizo letu la kukosa maendeleo. Ni kwa nini suala la umataifa wa istilahi liwe muhimu kwa lugha za mataifa yanayoendelea tu? Ni kwa kiwango gani lugha nyingine ulimwenguni zinajali maslahi ya wazungumzaji wa lugha za Kiafrika katika upanuzi wao wa istilahi? Suala la umataifa katika istilahi za Kiswahili lahitaji makini zaidi. Uendelezaji wa lugha ya Kiswahili sharti uyaweke mbele maslahi ya watumiaji wa lugha hii. Kwa maana hiyo, iwapo umataifa unalengwa kuhakikisha kuwa istilahi mpya inafaa kwa watumiaji wote wa Kiswahilii ndani na nje ya nchi ilimoundwa, basi ni sawa. Lakini kama tutauelewa umataifa kumaanisha jamii

ya binadamu ulimwenguni kote tutakosea. Mbona dhana mpya zinapopata msamiati katika lugha ya Kiingereza tunaupokea tena bila maswali? Vivyo hivyo, tunautarajia ulimwengu kuamini maamuzi yetu kuhusu msamiati wa kueleza dhana mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.

Isitoshe, labda suala la umataifa lina umuhimu zaidi katika taaluma za kiufundi, kisayansi, kitiba na kiteknolojia. Sidhani ni katika nyanja zote za matumizi ya lugha. Hebu tuzingatie mfano wa lugha ya Kijapani. Katika ustawi na uendelezaji wa lugha hiyo, ulifikia wakati wahusika wakakataa istilahi zenye asili ya lugha za kimagharibi na badala yake kutafuta katika lugha zao. Ilipokosekana, walitafuta katika lugha za Kichina na iliposhindikana wakakopa kutoka lugha za nje lakini hili lilikuwa tukio nadra sana. Kwani hivi sasa Kijapani hakina hadhi na nafasi nzuri katika ngazi ya kimataifa kwa kukosa msamiati mwingi wa kimataifa? (ambao kwa wengi ni sawa na msamiati wa Kiingereza) Ilivyo, kuhusu suala la umataifa wa istilahi, msisitizo umekuwa wa kutohoa kutoka kwa Kiingereza (Mbaabu, 1989; na Mwansoko, 1990). Kwa mfano, BAKITA imelaumiwa kwa kusisitiza istilahi za Kiingereza na kupuuza nyingi zinazozalishwa na kupendekezwa na wataalamu wa isimu (Mwaro, 2000). Kigezo cha umataifa hakipaswi kutufunga hata kidogo. Nadhani suala kuu hapa ni kuwa tumeamini ni vizuri kukopa kutoka lugha 'kubwa' na wala si kwamba lugha ya Kiswahili haiwezi kujitosheleza.

**Utetezi wa Mumo kwa Mumo**

Tunapoipendekeza lugha ya Kiswahili kuchukua nafasi muhimu katika ngazi za kitaifa na kimataifa, aghalabu tunataja kuwa miongoni mwa sifa zake kuu ni uwezo wake wa kupanua msamiati na kuzieleza dhana mbalimbali zinazoibuka. Itakuwaje tena sisi haohao tuonyeshe mtazamo tofauti kabisa kwa kuchukua tu maneno ya kigeni? Si hilo ni kinyume kabisa cha hizo kauli zetu?

Uchunguzi wa Mdee (1980) kuhusu ukubalifu wa msamiati wa biashara na wa ofisi katika mji wa Same-Mkoani Kilimanjaro, japo haukuzingatia mbinu zote za uundaji wa istilahi, ulihitimisha kuwa mbinu ya kuendeleza Kiswahili kiistilahi mumo kwa mumo ndiyo inayounda istilahi zenye ukubalifu mkubwa sana kwa walengwa. Ilijitokeza kuwa mbinu bora. Kuhusu uwanja wa isimu, Mwaro (2000:131-2) anasema hivi:

> Istilahi za isimu ya Kiswahili zinazoundwa kutokana na mbinu ya unyambuaji hueleweka kwa urahisi na walengwa na watumiaji wa Kiswahili kwa sababu hunyambuliwa kutokana na mizizi ya Kiswahili chenyewe.

Kwingineko, Mwaro (2000: 303, amemnukuu Mdee, 1986) akisema kuwa:

> Kiswahili kina maneno mengi asilia ya kuweza kueleza dhana kadhaa, lakini kutoyajua kwetu kumetufanya kuunda au kutohoa maneno kwa dhana hizo.

Huo ni ukweli kabisa ila tatizo ni kwamba baadhi ya wahusika hawataki kukubali kuwa maneno yapo, kwani hawayajui. Aidha, kutoyajua kwetu hakupaswi kuwa kikwazo kwa sababu Waswahili wapo wawezao kutuauni. La kuzingatiwa ni umuhimu wa kuwa tayari kushirikiana katika harakati zetu za kubuni istilahi za Kiswahili. Mdee anashauri ifuatavyo:

> waunda maneno hawana budi kudurusu kamusi za Kiswahili (za zamani) ili wayafahamu maneno mengi ya Kiswahili wasiyoyajua ambayo wangeweza kuyatumia kueleza dhana mpya badala ya kutohoa au kuunda neno jipya (nukuu katika Mwaro, 2000: 356).

Aidha, Mwaro (2000:135) anawataja wataalamu wengi mfano, (Mwansoko 1990, 1996; Goetschalckx 1989; Tumbo-Masabo na Mwansoko 1992 na Bwenge 1996), wanaoshikilia msimamo sawa kuwa mbinu ya uambatanishaji ni zalishi, huunda istilahi angavu na zinazoeleweka na walengwa kwa urahisi. Isitoshe, kulingana na tathmini ya Mwaro (2000) iliyozingatia vigezo vya PEGITOSCA, kwa kuzingatia istilahi 70 za isimu ya Kiswahili, istilahi zilizoundwa kutokana na uasilishaji kutoka Kiswahili chenyewe zina 'usayansi' zaidi, na zile zitokanazo na kukopa na kutohoa hazina 'usayansi' hata kidogo. Kama hali ni hii, kwamba mbinu kadhaa zinazotumia lugha ya Kiswahili chenyewe zinaunda istilahi zinazokubalika na kueleweka kwa urahisi, ni kwa nini tuendeleze mazoea ya kukopa maneno mengi ya Kiingereza? Je, Kiswahili kimeishiwa katika unyambuaji na uambatanishaji? Jungu limekosa ukoko kweli? Sidhani hivyo. Malighafi ipo; yaani lahaja mbalimbali za Kiswahili pamoja na lugha nyingine za Kibantu na kinachohitajika ni kiwango cha juu zaidi cha ubunifu, kutoka kwa wataalamu wa lugha ya Kiswahili. Itokeapo kuwa hilo haliwezekani katika baadhi ya dhana (nadhani hii itakuwa nadra mno), basi Kiingereza au lugha nyingine iwe changizi lakini istilahi husika iswahilishwe kwanza kabla ya kuingizwa katika msamiati wa Kiswahili.

Kuna imani kuwa tofauti ya mtazamo kuhusu suala hili, inabainika katika misingi ya kimaeneo. Kwa kiasi kikubwa, wataalamu wa Kenya (mfano, Nabhany, 1982; Mbaabu, 1995; na Chimerah, 1998), wanapendelea zaidi ukuzaji wa Kiswahili kwa kurejelea lahaja zake, tofauti na Watanzania wengi wanaoelemea zaidi lugha za kigeni, husuan Kiingereza. Mathalani, Massamba

(1996, katika Mwaro, 2000), anasema kuwa hakuna haja ya kutumia runinga ilhali televisheni limeishazagaa na kuenea. Sidhani kuwa hiyo ni sababu tosha kwani kwa kawaida lugha hubadilika na mabadiliko hayo ni pamoja na kurekebisha palipotokea makosa. Madai haya yanahitaji uchunguzi zaidi ili yatolewe kauli thabiti. Ni bora ifahamike kama ni kweli kuwa kuna tofauti kimaeneo na kama ipo ni kwa sababu gani?

Ingawa ni kweli kuwa lugha nyingi hukopa msamiati, wataalamu wa lugha nyingi wameanza kuepukana na utaratibu huu wa kupanua leksikoni za lugha zao. Lugha kadhaa, kwa mfano Kijerumani, zinajaribu kurutubishwa kwa kuhimizwa matumizi ya istilahi asili badala ya mikopo (Coulmas, 1982). Nyingine kama Kiarabu, Kiebrania, Kijapani, Kikorea, pamoja na Kichina (Mwaro, 2000), kwa sasa, hazionei fahari istilahi za mkopo bali hujikita zaidi katika lugha asilia. Sidhani kuwa twaweza kudai kwamba lugha hizi hazijaendelea ama mataifa yanayozitumia hayajaendelea kisayansi na kiteknolojia kwa sababu hazielemei Kiingereza. Aidha, hatuwezi kamwe kudai kuwa lugha hizi zina matatizo katika mawasiliano ya kimataifa kwa sababu zinajaribu kujiendeleza mumo kwa mumo. Ni kwa nini sisi pamoja na mataifa mengine ya Kiafrika tunaendeleza msimamo usiokuwa na msingi kwamba bila Kiingereza hakuna maendeleo? Pamoja na ukweli kuwa idadi kubwa ya Wachina, Wakorea na Wajapani hawajui Kiingereza, nchi hizo si zimeendelea kuzidi nchi nyingi zitumiazo lugha ya Kiingereza?

Ni lazima pia ikumbukwe kuwa kuingiza istilahi nyingi kupindukia kutoka lugha za kigeni kunaweza kuwa na athari hasi katika lugha ya Kiswahili, ikiwa ni pamoja na kusababisha mabadiliko katika muundo wa kisarufi. Lugha ya Kiindonesia imekumbwa na hali hii kutokana na kupokea istilahi nyingi za kigeni. Pili, kunakuwa na visawe vingi mno, hali ambayo inakanganya watumiaji wa lugha. Tatu, ni swala la tahajia; yaani istilahi mkopo zafaa kuandikwa vipi zinapoingizwa katika Kiswahili? Je, viambishi vya istilahi vitoholewe ama vitafutiwe visawe vyake vya Kiswahili? Kwa sasa, yote mawili yanafanyika. Binafsi, ninapendelea ushauri wa awali wa BAKITA (Kakulu, 1982). Isitoshe, tukizingatia suala la uundaji wa msamiati na uendelezaji wa lugha kwa mapana yake; ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kujaribu kuhifadhi asili ya lugha ya Kiswahili, huo ndio utaratibu mwafaka zaidi.

**Mchango wa Mwaro**

Suala la uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kupitia uundaji wa msamiati limeshughulikiwa na Mwaro katika maisha yake yote ya kisomi. Lakini siyo yeye pekee ambaye hili limekuwa eneo lake la kitaaluma. Wapo watafiti na wasomi wengi sana wa lugha ya Kiswahili ambao wametoa mchango si haba katika uundaji wa istilahi za Kiswahili. Lakini, katika kulishughulikia, Mwaro

ameyazamia zaidi baadhi ya mambo ambayo yalikuwa hayajafafanuliwa sana. Kwa kufanya hivyo, ameacha mchango muhimu katika uwanda wa leksikografia ya Kiswahili. Mahsusi, mwalimu Mwaro ametoa mchango ufuatao.

Tofauti na waliomtangulia (kwa mfano, Ohly 1972; Mdee 1980; Nabhany 1982; Kapinga 1983; Mbaabu 1985; Mwansoko 1990; Tumbo-Masabo 1990, na Tumbo-Masabo na Mwansoko, 1992), amabao kwa kiasi kikubwa walikuwa wanaishia tu kuzieleza mbinu mbalimbali za uundaji wa istilahi kisha kutoa mifano ya maneno yaliyoundwa kufuatia mbinu hizo, Mwaro (2000), amelizamia zaidi suala hili la mbinu za uundaji wa istilahi kwa kuzitolea ufafanuzi mpana. Yeye mwenyewe anasema hivi:

> Maelezo ya wataalamu hawa wote ya mbinu za kuundia istilahi za Kiswahili, hata hivyo, yalielekea kuwa ya 'kijumlajumla'. Mtindo ulikuwa ni kutaja mbinu zote za uundaji wa istilahi za Kiswahili, na kutoa mifano michache ya istilahi zilizotokana na kila mojawapo ya mbinu hizo. Sisi tulitathmini istilahi za isimu ya Kiswahili na mbinu za uundaji istilahi hizo ili kuona kama zinazingatia usayansi, na wakati huo huo, ni mbinu ipi inayounda istilahi zenye usayansi, zilizo faafu, na zinazosadifu zaidi kimataifa (2000:4).

Kwanza, amefafanua tofauti iliyopo baina ya mbinu ya unyambuaji na uambishaji katika uundaji wa istilahi za Kiswahili, ambazo wataalamu wengi awali walikuwa wanazijadili kwa pamoja; amebainisha wazi zaidi mbinu za akronimu, uhulutishaji, na ukatizaji kama mbinu za ufupishaji (kwa pamoja) za kuundia istilahi; na amedokeza dosari katika baadhi ya mbinu zinazotumika kuundia istilahi za Kiswahili. Kwa mfano, ameonyesha kuwa hakuna kanuni maalum zinazoongoza uundaji wa istilahi kutumia mbinu ya uhulutishaji (Mwaro, 2000:144-45).

Katika kuijadili mbinu ya upanuzi wa maana ya maneno, Mwaro (2000: 148-50), anahitimisha kwa kusema kuwa mara nyingi istilahi zinazoundwa zinakosa uangavu na hutatanisha walengwa. Hata hivyo mifano anayoitoa, kwa maoni yangu, si upanuzi wa maana bali ni ubadilishaji wa maana kabisa. Kwa mfano, neno la Kiingereza "lust" ambalo awali lilimaanisha furaha na utashi halitumiki kwa maana hiyo kabisa hivi sasa bali maana ya uzinifu ndiyo imekita zaidi. Vivyo hivyo kwa "garbage" na "rent."

Yeye amejitokeza kama mtetezi wa mbinu ya ufufuaji, anayoieleza kama kurudisha katika matumizi msamiati au istilahi ambazo hazikufikiriwa katika Kiswahili sanifu. Wataalamu wengi wanaounga mkono mbinu hii wanasema kuwa kuijenga lugha ndani ya lugha ndiko kuikuza lugha. Aidha, ameitolea mbinu hii ya uundaji wa istilahi ufafanuzi wa kina inaoustahiki. Awali ya hapo,

wataalamu wengi walioizungumzia, kama vile Abdulaziz (1989), Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992), Bwenge (1996), Sewangi (1996), pamoja na Chimerah (1998), waliipitia kwa juujuu bila kuizamia.

Vilevile, Mwaro amelizamia kwa kina zaidi swala la matatizo yanayotokana na ukopaji wa istilahi kutoka kwa lugha za kigeni, hasa ya Kiingereza. Hapa napo, wataalamu waliokuwa wameligusia awali (mfano, Tumbo-Masabo, 1990; Chuwa, 1988; na Massamba, 1996) hawakuwa wamelijadili kwa mapana na marefu. Matatizo ya msingi yaliyofafanuliwa ni: namna ya kuzitamka; jinsi ya kuziandika; mpangilio sahihi wa maneno, na namna ya kuvishughulikia viambishi na maumbo unganifu ya kisayansi.

Kwa jumla, Mwaro (2000:111) anakubaliana na msingi uliotolewa na BAKITA( Kakulu, 1982 ) wa kuanzia lahaja za Kiswahili, lugha nyingine za Kibantu, na kuswahilisha zile za kigeni, na yote hayo yasipofaulu, istilahi mpya ziundwe kwa kuzingatia misingi ya kisayansi ya kuunda istilahi. Akiitongoa misingi inayofaa kufuatwa katika uundaji wa istilahi za Kiswahili, kuhusu kanuni ya C katika vigezo vya PEGITOSCA, anasema hivi:

> Upanuaji kimaana wa istilahi zenyewe za Kiswahili, na matumizi ya istilahi asilia pale ambapo hapana neno mwafaka, uendelezwe Mwaro (2000:90).

Anatoa mifano ifuatayo:

1. "x-ray"== uyoka badala ya eksirei.
2. "blood pressure"== buhari badala ya presha au mtuto wa damu.
3. "focus"==viwendu badala ya fokasi.
4. "leave"==sono badala ya livu au mapumziko.

Ninakubalina na haya mapendekezo yake ya msamiati lakini tofauti naye, badala ya kutumia msamiati asilia pale ambapo hakuna neno muafaka, twapaswa kutumia neno la kigeni pale ambapo hakuna neno muafaka la kiasili. Tuanzie ndani na tukosapo neno muafaka ndipo tutoke nje.

Vilevile, anapendekeza kuwa uundaji wa istilahi kwa kutumia lahaja za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu uendelezwe. Mifano aitoayo ni:

1. "television"==runinga badala ya televisheni
2. "radio"==bomba/mwengoya badala ya redio
3. "science"==ulimbe (sayansi)
4. "mathematics"==maenga (hesabu)

Hii ndiyo mbinu ambayo ingepaswa kupata kipaumbele kila mara panapozuka umuhimu wa kuunda istilahi mpya. Ni baada ya kukosa kabisa

istilahi muafaka kutokana na vyanzo hivi ambapo twaweza sasa kugeukia lugha nyingine. Ipo mifano ya lugha nyingine ulimwenguni ambazo zimetumia mbinu hii ya kuunda istilahi na kuiendeleza lugha mumo kwa mumo. Hizi ni pamoja na Ufini na Uswidi, Indonesia na Malaysia, China na Japani, Uyahudi na kadhalika. Aidha, kwa sababu ya kutaka kujenga utaifa, istilahi asilia za Kiebrania zilifufuliwa na zingine mpya kuundwa kwa misingi ya lugha hiyo yenyewe (Mwaro, 2000 akiwarejelea Abdulaziz, 1989; Rabin, 1989 na Mwansoko, 1990).

Kwa jumla, Mwaro ametoa mchango mkubwa katika eneo la uundaji wa istilahi za Kiswahili kwani ameziendeleza mbele. Ni matarajio yangu kuwa wataalamu katika eneo hili watazirejelea kazi zake, hasa tasnifu yake ya uzamifu, "Usayansi wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili" ili kufaidi mawazo mema yaliyomo. Lakini, labda mchango wake mkubwa ni msisitizo aliotoa kwa umuhimu wa kuzingatia usayansi katika shughuli nzima ya uendelezaji wa msamiati wa Kiswahili. Anasema mbinu yoyote inayoteuliwa kutumiwa na asasi ama mtu binafsi ifuate kanuni na taratibu maalum. Usayansi huu utawezesha wataalamu wa lugha kuchunguza na kuzipima istilahi zinazobuniwa, kufuatia misingi hiyo, na kufikia uamuzi bora kuhusu kufaa ama kutofaa kwake. Aidha, hali ya ama kuzitetea au kuzipinga istilahi maalum bila kutoa sababu nzuri za kufanya hivyo, itaepukwa.

**Mkondo wa Kufuata**

Mwansoko (1990), anapendekeza kuwa ni bora istilahi ziundwe kulingana na kiwango cha elimu cha watumiaji wa lugha. Sidhani kuwa kuna ulazima wowote wa kuwa na makundi mawili ya istilahi katika uwanja wowote wa matumizi ya lugha. Mwaro (2000) anasema, hilo litawakanganya zaidi watumiaji wa lugha. Mtu hahitaji kuwa msomi kuimudu lugha yoyote iwayo. Mbona lugha nyingine ulimwenguni hazina makundi tofauti ya msamiati? Wazee wengi wa Kiafrika waliopigana katika vita vikuu vya dunia walirudi wakiwa na msamiati, japo finyu, wa lugha ya Kiingereza. Ukweli kuwa walikuwa hawana elimu haikuwazuia kuyapata hayo maneno machache ingawa walitatizika katika matamshi. Walijua 'bloody fool' ni mjinga ijapokuwa hawakulitamka vilivyo (namjua mmoja anayelitamka 'bilari furu'). Kwa hiyo, wanaohusika waunde istilahi na wazieleze kwa uwazi kwa umma na zitatumika tu. Watu wengi hivi sasa wanatumia istilahi ya utandawazi hata kama baadhi hawaijui vizuri dhana ya utandawazi. Nchini Kenya, neno tarakilishi linatumiwa na watu wengi ikiwa ni pamoja na ambao hiyo tarakilishi hawajawahi kuiona. Kwa kifupi, wanaohitaji kujadili mada za kitaaluma zaidi watatumia istilahi za kitaaluma ilhali wengine watatumia msamiati wa kawaida kulingana na mahitaji yao mbalimbali.

Kulingana na nadharia ya istilahi ya NJI, dhana mpya zainapoingia katika jamii-tumizi-lugha au sehemu ya jamii, zinafaa kukopwa pamoja na istilahi zake (Mwansoko, 1990:129). Lakini ni lazima iwe hivyo wakati wote? Nadharia yapaswa kuwa mwongozo wala haipaswi kutufunga katika harakati zetu za kuikuza lugha. Lugha ya Kiswahili, japo imevuka mipaka na kuwa ya kimataifa, ni yetu mwanzo na maslahi yetu ndiyo yanapaswa kuwekwa mbele. Isitoshe, imebainika kwamba si nadharia na kanuni zote zitokazo ughaibuni ni nzuri kwa mazingira yetu. Hili limebainika wazi, kwa mfano, katika nyanja za uchumi na siasa, ambapo mataifa yanayoendelea yamelazimishwa kufuata mifumo ya kimagharibi, bila kujali mazingira tofauti yaliyo nyumbani, matokeo yake yamekuwa kinyume na hali iliyotarajiwa. Ni lazima tuzitazame kanuni zilizopo kwa kuzihusisha moja kwa moja na hali halisi katika mazingira yetu. Tuchukue yanayotufaa na kuacha yasiyotusaidia. Sidhani kwamba kukopa dhana na istilahi zake itaisaidia lugha ya Kiswahili hata kidogo. Kwa sababu hiyo, nakubaliana zaidi na msimamo wa nadharia ya istilahi za kisayansi inayoshikilia kuwa dhana mpya zinapoingia katika jamii, zinafaa kukopwa lakini si pamoja na istilahi zake. Zikopwe na kuundiwa istilahi muafaka (Mwaro, 2000). Dhana ni za kimataifa lakini istilahi si lazima iwe ya kimataifa. Matumizi ya istilahi za kiasili, nadhani, yanasaidia kuifanya dhana husika ieleweke na kuingia katika mfumo wa maisha wa wahusika kwa urahisi zaidi. Kwa kawaida, kutokana na imani uliyonayo kwa wasomi na wataalamu wake, umma huwa tayari kuupokea msamiati unaobuniwa. La kufanywa ni kuwahi kuzitafutia dhana mpya msamiati wa kiasili na ulio muafaka. Hili likifanyika, watumiaji wa lugha hawatakataa kuutumia msamiati huo. Ndipo *mtandao*, *tovuti*, *tarakilishi*, *utandawazi* na mengineyo yamekubalika na hutumika.

Akizieleza baadhi ya dosari za nadharia ya jumla ya istilahi, Mwaro (2000: 45) anaukosoa mtazamo wake wa kusisitiza kuwa dhana mpya zinapoingia katika lugha na istilahi zake ziingie pia. Anasema kuwa mtazamo huo hautambui ubunifu katika lugha; ubunifu ambao tumesema wakati wote kuwa ni miongoni mwa nguvu ya Kiswahili. Lakini huenda Wuster na wengine kama yeye walikuwa na nia maalumu ya kusisitiza hivyo. Mataifa ya kimagharibi mara nyingi hutaka mataifa yanayoendelea kufuata yanachokifanya. Ni vizuri kwao tuendeleapo kukopa istilahi za lugha zao mbalimbali moja kwa moja kwa sababu kadhaa. Kwanza, tutaendelea kuwategemea wao. Pili, watapata silaha zaidi za kuzipiga vita lugha zetu kwa madai kuwa lugha hizo hazijitoshelezi na haziwezi kumudu mawasiliano ya kisiku hizi. Mataifa ya Kiasia yamefaulu kuzilinda lugha zao kwa kiasi kikubwa na sasa, kwa sababu ya mafanikio yao kimaendeleo, Wamarekani, Waingereza na wazungu wengine hulazimika kujifunza lugha za Kijapani, Kichina, na Kikorea kwa sababu za kiusalama, kiuchumi, na kadhalika. Mataifa hayo ya Kiasia hayakujali kama lugha zao

zitatizamwa kuwa za kimataifa au la. Vivyo hivyo, watakaoihitaji lugha ya Kiswahili watajifunza tu, na kwa hakika tayari wanajifunza. Hatuhitaji kulijali hilo. Tuwajali watu wetu ambao ndio watumiaji wengi wa lugha ya Kiswahili.

> ……katika nadharia jumla ya istilahi, istilahi zilizozoeleka, au zilizozagaa na kuenea katika fahamu za watu kwa muda mrefu hazipaswi kupembuliwa na kubuniwa istilahi mpya mahali pake (Mwaro, 2000:41).

Hali hii inamaanisha kuwa ni muhimu sana kuhakikisha kuwa dhana mpya inapoibuka katika jamii suala la istilahi muafaka ya kuirejelea linazingatiwa mara moja. Hilo lisipofanyika, kutokana na uhitaji wa kuishirikisha dhana hiyo katika maisha yao, watumiaji wa lugha wataipatia istilahi tu, iwe muafaka au la. Kwa hakika, uhitaji huu wa kuendeleza mawasiliano ni miongoni mwa sababu kuu ya kujitokeza kwa istilahi ambazo baadaye wataalamu wanazikataa kwa kukosa ufaafu. Watumiaji wa lugha, pamoja na ukweli kuwa wana ubunifu wa hali ya juu, wanahitaji kuongozwa, na hilo ni jukumu la wanaistilahi.

Licha ya ukweli huo, hakuna sababu ya msingi kusisitiza kuwa istilahi iendelee kutumika kwa sababu imeishazoeleka miongoni mwa watumiaji wa lugha. Iwapo utafiti umeonyesha kuwa istilahi maalum ina makosa basi na irekebishwe. Jinsi ambavyo hiyo ya awali ilizoeleka ndivyo na hiyo mpya itakavyozoeleka. Haidhuru kama itachukua muda. Kwani tuna haraka ya kwenda wapi? Ikiwa kosa hilo halitarekebishika kabisa wakati huu, tuyaanze marekebisho hayo na wayafaidi watoto au wajukuu wetu baadaye.

Kufuatia nadharia za uundaji wa istilahi, kuna kanuni maalum zinazoongoza wahusika. Kaida hizi zinapofuatwa, wahusika wanaweza kuibuka na istilahi zinazoakisi mahitaji ya lugha, na zinazokubalika kimataifa. Aidha, ni muhimu istilahi hizo zikubalike na watumiaji wa lugha husika. Miongoni mwa sifa muhimu ya kufikiriwa, anavyosisitiza Mwaro (2000: 64) ni dhana ya usayansi, inayohitaji istilahi kufanyiwa majaribio ili kuona kama imefuata kanuni muhimu na kama inakubalika. Hali hii itazifanya zitumike kwa ulinganifu (bila kubadilishwabadilishwa). Aidha, istilahi kama hizo hupata kusanifishwa na hivyo kutumiwa na wahusika wote kwa maana moja (Felber 1984, akinukuliwa na Mwaro, 2000: 64). Lakini shughuli ya uundaji wa istilahi si rahisi. Licha ya haya yote kuzingatiwa na wanaistilahi wa Kiswahili, bado kuna manung'uniko kutoka kwa watumiaji wa lugha hii. Aidha bado kuna istilahi zitumikazo ambazo kwa baadhi, hata kama hawajalalamika waziwazi, zinaitia doa lugha ya Kiswahili.

Ieleweke wazi kuwa wengi tunatambua juhudi za muda mrefu za mashirika mbalimbali, kama vile BAKITA, TUKI, na kadhalika, pamoja na watu binafsi katika uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kwa kubuni msamiati. Ndiyo sababu

Kiswahili kimetufikisha tulipo, tena kwa fanaka isiyo kifani, kutokana na jitihada za wapenzi hao wa lugha. Kuna dhana nyingi ambazo zimebuniwa istilahi katika vipindi tofautitofauti na zikakubalika na kuingia katika matumizi moja kwa moja na kwa urahisi. Baadhi hazikukubalika kwa urahisi na labda hata zimebakia kutumiwa na wachache tu. Hata hivyo, katika makala haya, sitajishughulisha na hizo zilizokubalika bali katika sehemu hii nitatoa mifano ya istilahi ambazo, kwa maoni yangu, tunailazimishia lugha ya Kiswahili bila sababu ya kufanya hivyo. Japo zinakubalika na kutumika, kwa maoni yangu zinachangia kuiondoa lugha hii kutoka kwenye uasili wake. Mifano hii inalenga zaidi katika kuonyesha kukithiri kwa mazoea ya kupendelea mbinu ya kukopa maeneno ya kigeni (Kiingereza zaidi) na kuyabadilisha moja kwa moja (kuyaswahilisha) yalivyo.

Maneno yaliyo katika orodha A yana upungufu gani (yamekosa kukidhi mahitaji gani) mpaka tuanze kutumia yaliyo katika B?

| A | | B |
|---|---|---|
| Ukatibu | - | sekretariati |
| mtuto wa damu | - | presha |
| chano au sinia | - | trei |
| kiimbo | - | intonesheni |
| awamu | - | fezi |
| chembechembe | - | seli |
| kiwakilishi nomino | - | pronomino |

Maneno mengine ni pamoja na *agronomia, saikatria, prediketa, aspekti, sabfamilia, stredenti, anteria, spishi, nazali*, na kadhalika (Mwaro, 2000). Mifano mingine nitaitoa kwenye kitabu cha Senkoro (2003), *Tuseme Kiswahili*. Nadondoa kutoka katika kitabu hiki, si kwa sababu ndicho cha pekee kinachotumia msamiati wa aina hii, bali kwa sababu ninakitumia kufundishia wanafunzi wa Kiswahili katika chuo kikuu cha St. Lawrence nchini Marekani. Aidha, ni ithibati kuwa msamiati huu unatumika katika machapisho rasmi ya wakati huu. Mifano ni mingi ila hii ifuatayo itatosha kwa minajili ya kuifafanua hoja hii. Pale ambapo tayari kuna msamiati ninaodhani ni muafaka zaidi katika lugha ya Kiswahili, nimeuweka katika mabano: *yunifomu* (sare), *baamedi* (mhudumu), *nesi* (muuguzi), *i-meli/barua*-e (baruapepe), *sefu* (salama), *geti* (lango), mataa ya *trafiki* (mataa ya barabarani), *kiplefti* (mzunguko), *fleti* (nyumba ya ghorofa), *begi* (mfuko) na kadhalika. Isitoshe kwa nini basi isiwe *flati* badala ya *fleti* na *bagi* badala ya *begi*? Ukiipitia *Kamusi ya Tiba* (2003) ya TUKI, utaona kuwa msamiati mwingi umetokana na mbinu hii, kwa mfano:

**aortitis** *n* aotitisi: inflamesheni ya mshipa wa aota
**lymphocytopenia** *n* limfositopenia
**macropsia** *n* makropsia

Lakini katika kamusi hiyohiyo, ipo mifano inayoonyehsa kuwa lugha ya Kiswahili yaweza kubuni msamiati wa kiasili kueleza dhana mbalimbali katika uwanja wa tiba. Kwa mfano:

**exsanguinate** *v* poteza damu
**extrovert** *n* msondani
**insemination** *n* uhamilishaji
**insecticide** *n* viuatilifu

Kama yawezekana, kwanini tusifuate mfumo huo zaidi badala ya ule wa kukopa moja kwa moja?

Yapo maneno mengine mengi ambayo tunakumbana nayo katika matumizi ya kila siku ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, matumizi ya maneno 'feli ' na 'pasi'. Nimekua nikijua kuwa mtu hupita ama kuanguka mtihani. Baadaye, nikaanza kusikia matumzi ya feli na pasi kwa maana hiyohiyo. Ni wakati gani watumiaji wa Kiswahili waliona msamiati pita na anguka hautoshi kueleza hali hizo na kuamua kutohoa 'fail' na 'pass'. Neno la Kiingereza la 'jubilee' limetoholewa kuwa jubilii katika *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili* (TUKI, 1996). Ni kwa nini tunatumia 'jubilei' (tazama mawasiliano ya TUKI kuhusu maandalizi ya sikukuu ya ukumbusho wa miaka 75 kwa mfano). Maneno mengine katika kundi hili, mengi ambayo nimeyasikia katika vyombo vya habari, ni pamoja na: *protokali* (itifaki), *komunike* (taarifa au taarifa ya pamoja), *hafukasti* (chotara), *waranti* (hati), *laivu* ( fuma, fumania) na kadhalika. Mifano mingi zaidi inapatikana katika vyombo vya habari vya Afrika Mashariki, zaidi katika magazeti ya Kiswahili nchini Tanzania.

Msamiati unaoundwa namna hiyo umekuwa mwingi mno katika lugha ya Kiswahili. Umefika wakati wa kujiuliza kama ni lazima tuendelee kufanya hivyo. Iwapo hapo awali wataalamu wetu waliitumia mbinu hii zaidi si umefika wakati wa kubadili mtindo? Hatuoni kuwa tukiendelea hivi lugha hii itaendelea kupoteza uasili na Uafrika wake? Mtindo huu unanikumbusha alichowahi kusema marehemu Jay Kitsao kuwa "kama mtindo ni huu, kwanini tusumbuke kusema habari za asubuhi? Si tuseme gudimoningi?" Sidhani tunataka kufika hapo.

Kwa bahati mbaya, baadhi ya wataalamu huzipuuzia mbali istilahi zinazobuniwa na wenzao bila hata kuzitathmini. Si ingekuwa bora kufanya tathmini ya kina, na inapowezekana hata kupata maelezo kamili kutoka kwa

mbunaji badala ya kuharakisha kuidunisha istilahi? Wapo pia ambao hujali zaidi istilahi ilibuniwa wapi (Kenya au Tanzania), na ni nani (au chombo gani) aliyeibuni badala ya kujali ubora wa istilahi yenyewe. Kwa mfano, neno 'umenke' lililopendekezwa na Chimerah lilihukumiwa na wasomi wengi kwa namna hii. Tatizo jingine ni kwamba, kutokana na mazoea ya kuegemea zaidi istilahi za mkopo kutoka lugha ya Kiingereza, liibukapo neno ambalo halifuati utaratibu huo, ambalo limetokana zaidi na ubunaji wa mwanalugha kwa mtazamo wa kutafuta katika Kiswahili chenyewe, wengi hulishuku. Isitoshe, kwa sababu TUKI na BAKITA ni vyombo rasmi, vina mamlaka fulani na watumiaji wengi wa Kiswahili huyakubali yatokayo kwa vyombo hivyo kwa urahisi tofauti na maneno yatokayo kwa wanaistilahi wengine. Ukweli ni kwamba si yote yatokayo katika vyombo hivyo yaliyo mazuri, na kwa sababu hii, inabidi vyombo hivi viwe makini zaidi kwani kupitisha istilahi zisizo muafaka kutaathiri lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa mno.

Kwa mfano tunaitendea lugha ya Kiswahili haki tunapoanza kutumia maneno kama *advebo* kuieleza "adverb" na *tipolojia* kuelezea 'typology'? Kuna shida gani kutumia kielezi? Sasa hiyo 'tipolojia' inafaa kutamkwa vipi? Matamshi yafuate Kiingereza ama Kiswahili? Kwa nini si taipolojia basi? Labda tuna sababu nyingine kabisa ambazo hatutaki kuzitaja wazi wazi. Iwapo itabidi tuendelee kuelemea zaidi mbinu ya ukopaji, kama ambavyo inafanya TUKI, basi ni bora tutumie kanuni za tafsiri ya maana badala ya utohoaji na kaleki. Matokeo yake ni maneno kama vile: *kifyonzo* (sibilant), *badili* (complimentarity), *msuguano* (friction) ambayo nadhani ni bora. Japokuwa Mwaro (2000: 239) anasema kuwa nyingi ya istilahi zitokanazo na kanuni hii hazina uangavu, nadhani ni bora kuliko; *elementi*, na *tagma* yatokanayo na hizo kanuni nyingine. Hayo ya tafsiri ya maana, kwa hakika, yanasomeka na kusikika kama maneno ya Kiswahili hasa.

**Hitimisho**

Uundaji wa istilahi ni jambo ambalo lugha zote ulimwenguni hukumbana nalo wakati wote. Haliwezi kuepukika. Sababu za hali hii ni nyingi na za msingi. Kwa mfano, ni kawaida kuwa binadamu, kila mara yuko mbioni kubuni dhana mpya katika juhudi zake za kutaka kuyatawala mazingira yanayomzunguka. Katika hali hiyo, na kutokana na maarifa mapya ya uvumbuzi, ni sharti istilahi mpya ziendelee kubuniwa. Kiswahili hakiwezi kuliepuka hili.

Hata hivyo, utatuzi wa suala hili la mbinu mwafaka za ubunaji wa istilahi za Kiswahili unahitaji makini zaidi. Kwa mfano, Mwaro (2000) anajitokeza kama mtetezi mkuu wa uendelezaji wa Kiswahili mumo kwa mumo, lakini wakati huohuo anaikosoa TUKI kwa kutumia msamiati ufuatao: ngozi nje = epidermis, kifasiri = gloss, faridipeke = particle, kinong'onwa = breathed segment,

utegemezi = hypotaxis na kadhalika. Sababu anayoitoa ni kuwa hawakuzingatia utaratibu maalumu wa uundaji, pamoja na umuhimu wa viambishi mkopo kuswahilishwa kwa utaratibu maalumu ili vijitokeze vizuri katika dhana mbalimbali zinazokaribiana kimaana (ulinganifu wa mtiririko). Lipi lipewe umuhimu wa kwanza? Huo ulinganifu wa mtiririko ama upunguzaji wa ugeni katika lugha ya Kiswahili? Ni sharti masuala haya yawekwe wazi zaidi ili tusiwe tunawakosoa wahusika kwa juhudi zao na wakati huohuo kuwakashifu tena wanapojaribu kuzingatia lugha asili. Kwa jumla, suala zima la uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kwa kuiundia msamiati mpya lahitaji kujadiliwa kwa mapana na kuwekewa mikakati bora. Sharti pawe na ushirikiano wa karibu zaidi baina ya vyombo, taasisi na watu binafsi wanaojishughulisha na uundaji wa istilahi ili juhudi zao zielekezwe katika lengo moja. Afrika Mashariki ina jukumu la kipekee la kuongoza dira ya uendelezaji wa Kiswahili. Hili lazima lifanyike kwa namna ambayo inailinda lugha hii. Ni lazima tuweze kuionea fahari na wala si kufanya pupa na baadaye kuijutia juhudi tutakayokuwa tumeifanya.

## Marejeo


Abdulaziz, M.H. (1985), "Aspects of Lexical and Semantic Elaboration in the Process of Modernization of Swahili", katika J. Maw na D. Parkin (wah.), *Swahili Language and Society,* Vienna, Afro-Publishers, 1952-213

Abdulaziz, M.H. (1989), "Development of Scientific and Technical Terminology with Special Reference to African Languages", katika *Kiswahili*, Juz. 56/1&2: TUKI, 32-49

Akida, H. (1977), "Kiswahili kama Lugha ya Kimataifa, Umuhimu wa Arki za Kiarabu", katika *Mulika,* Na. 11, Dar es Salaam: TUKI

Bwenge, C.M.T. (1986), "Utafutaji, Uundaji na Utumiaji wa Istilahi katika Tafsiri", katika *Mulika* Na. 23, Dar es Salaam: TUKI, 56-71

Chimerah, R.M. (1998), *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press

Chuwa, A.R. (1988), "Foreign Loan Words in Kiswahili", katika *Kiswahili*, Juz. 55/1&2, Dar es Salaam. TUKI, 163-172

Coulmas, F. (mh.) (1989), *Language Adaptation*. Cambridge: Cambridge University Press

Felber, H. (1984), *Terminology Manual*. UNESCO and Infoterm, Paris: INFORMTEM Series 21/Unisist

Gibbe, A.G. (1981), "Istilahi za Fonolojia: Tatizo katika Usanifishaji wa Lugha ya Kiswahili", Makala iliyowasilishwa katika Semina ya Pili ya Chama cha Fonolojia cha Tanzania, Dar es Salaam, Disemba 1981

Goetschalck, J. (1989), "Introduction-Terminology as a Tool", katika J. Jolly (Mh.), Proceedings of the North American Translators Congress, Washington, D. C.

Kakulu (BAKITA) (1982), *Kakulu 3*, Kamati ya Kusanifu Lugha, Dar es Salaam
Khamisi, A. M. (1987), "Trends in Swahili Lexicography", katika *Kiswahili*, Juz. 54/1&2, Dar es Salaam: TUKI
Kiingi, B.K. (1989), "A Systematic Approach to the problem of the Expressional Modernisation in the Formal and Natural Sciences: The case of Luganda", Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Bielefed
Kiputiputi, O.M. (1999), "Kwa nini Kiswahili Kinafaa kuwa Lugha ya Kufundishia Masomo ya Sayansi na Teknolojia", katika Z.N. Tumbo-Masabo na E.K.F. Chiduo (wah.), *Kiswahili katika Elimu*, Dar es Salaam: TUKI
Likhalo, P.I. (1991), "Ufaaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kisomo", Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.
Mac William, A. (1985), "Some Thoughts on Translation of Scientific Terminology in Kiswahili", katika *Kiswahili*, Juz. 52/2, Dar es Salaam: TUKI, 102-112
Massamba, D.P.B. (1996), "Problems in Terminology Development: The Case of Tanzania", katika *Kiswahili* Juz. 59, Dar es Salaam: TUKI: 86-98
Massamba, D.P.B. (1989), "Zoezi la Uundaji wa Istilahi katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili", katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI: 74-91
Mbaabu, I. (1989), "Ukubalifu wa Msamiati: Mifano kutoka Kenya", katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI, 23-28
Mbaabu, I. (1995), "Dhima ya Kamusi Katika Kufundisha na Kujifunza Kiswahili", Katika J.G. Kiango (mh.) *Dhima ya Kamusi katika Kusanifisha Lugha. Dar es Salaam:* TUKI, 47-59
Mc Crum, R., W. Cran & Mc R. Neil (1986), *The Story of English*. New York: Elizabeth Sifton Books, Viking Penguin Inc.
Mdee, J.S. (1980), "The Degree of Acceptability of New Swahili Words: Speakers' Response Analysis." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Mdee, J.S. (1983), "The Policy of Adapting Loan Words in Kiswahili as Conceived by BAKITA: A Critique", katika *Multiligua* Juz. 2/2. Mouton Publishers: 109-112
Mwansoko, H.J.M. (1989), "The Principles, Methods and Procedures of Swahili Terminology Development in Tanzania: A Re-examination of Basic Issues", katika *Journal of Asian and African Studies,* 38, 161-176
Mwansoko, H.J.M. (1990), "The Modernization of Swahili Technical Terminologies: An Investigation of the Linguistics and Litearture Terminologies", Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha York
Mwaro, G.A.W. (200), "Usayansi wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili", Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro, Kenya
Mwita, A.M.A. na Mwansoko, H.J.M (2003), *Kamusi ya Tiba*, Dar es Salaam: TUKI
Nabhany, A. S. (1978), "Kandi ya Kiswahili: Kamusi", Mswada (Haujachapishwa)
Nabhany, A. S. (1982), "Barua, Maoni, Mapitio, Mashairi..." katika *Kiswahili*, Juz. 49/2, Dar es Salaam: TUKI

Nkwera, F.V.M. (1978), *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Rabin, C. (1989), "Terminology Development in the Revival of a Language: The case of Contemporary Hebrew", katika F. Coulmas (mh.), *Language Adaptation*, Cambridge: Cambridge University Press

Senkoro, F.E.M.K. (2003), *Tuseme Kiswahili, A Multidimensional Approach to the Teaching and Learning of Swahili as a Foreign Language*, Madison: NALRC Press

Sewangi, S.S. (1996), "Ukubalifu wa Istilahi kwa Walengwa: Mfano wa Istilahi za Ufundi wa Matrekta/Magari" katika *Mulika* Na. 23, Dar es Salaam: TUKI, 12-23

Temu, C.W. (1984), "Kiswahili Terminology: Principles adopted for the Enrichment of the Kiswahili Language", katika *Kiswahili*, Juz. 51/1 na 51/2, Dar es Salaam: TUKI

Tumbo-Masabo, Z.N.Z na Mwansoko, H.J.M. (1992), *Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI